



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA



Watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya
Mbeya

05.04.2024

TANGAZO LA UTOAJI WA MIKOPO KUTOKA WIZARA YA FEDHA NA
MIPANGO

Sawa na kichwa cha habari hapo juu

2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya anawatangazia watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuwa amepokea mgao wa Fedha **TZS 400,000,000/=** kutoka kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango kwa watumishi wenye Sifa za kukopa na wenye uhitaji.
3. Utaratibu wa uombaji wa Mkopo husika kwa mwaka umebadilishwa hivyo watumishi wanaotaka kukopa wanatakiwa kujisajiri kwenye mtandao kwa kupitia **HAZINA PORTAL** kwa kuingia katika *google Chrome* <https://als.muse.go.tz> ndipo wataweza kuomba mkopo husika.


Vigezo na masharti kwa waombaji;

- i. Awe Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya
- ii. Makato ya Mshahara yasiwe yamefikia 1/3 ya Mshahara wake
- iii. Mshahara wake lazima awe analipwa kupitia Serikali Kuu (**HAZINA – At Source**) na awe na Cheki Namba
- iv. Awe ameajiriwa kwa Masharti ya Kudumu na Pensheni
- v. Mtumishi ambaye alishawahi Kukopa Mkopo huu wa Hazina kabla na ikiwa haujaisha hawezi kukopeshwa kwa sasa mpaka atakapo rejesha wote
- vi. Mkopo utarejeshwa kwa kipindi kisichozidi miezi 72 (Miaka Sita)
- vii. Mtumishi atakatwa 3% ikiwa ni kwa ajili ya kodi ya huduma na 1% kwa ajili ya **BIMA** ya Mkopo ambapo vyote hukatwa wakati anaingiziwa fedha husika kwa mkopaji
- viii. **Mtumishi anayeomba mkopo huu ni lazima awe amethibitishwa kazini hivyo ajira mpya hawatakiwi kuomba mkopo husika**
- ix. **Mtumishi mwenye mashauri ya kinidhamu hatakiwi kuomba Mkopo huu**
- x. Unapojisajiri hakikisha unakuwa na Anwani ya barua pepe (e-mail) ambayo inatumika na unaikumbuka Nywila yake, pia uwe na Namba ya Simu

- xi. Ukiwa unajisajili kwenye mfumo huu wa HAZINA PORTAL account ni lazime iwe ya mshahara unakopitia
- xii. **Mwisho wa Kupokea Maombi haya ni Tarehe 14.04.2024**

4. Kwa watumishi wenye uhitaji na watakaoshindwa kujisajiri katika anuani tajwa wafike katika jengo la Halmashauri ukumbi mkubwa
Mnamo tarehe 09.04.2024 kuanzia saa 9:00Asubuhi kwa ajili ya maelekezo ya namna ya kujisajiri na kuomba mkopo husika

5. Kwa mawasiliano kuhusu Mkopo unaweza kuwasiliana na Mratibu wa Mkopo Ndg. Sitti Nyerenga (Afisa Utumishi) kupitia Namba ya Simu 0755571042 na Gwakisa (Afisa Tehama) Namba ya Simu 0717140506



Aliko Mbuba

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
Mbeya

**¶ n.y. Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya**